JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO

MUHTASARI WA UTARATIBU WA KUHAMISHA KWENYE MAKAZI MAPYA (RFP) KWENYE UTEKELEZAJI WA MRADI WA TANZANIA YA KIDIJITALI (DTP)

Maelezo ya Awali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (WUUB) inaandaa Programu inayopendekezwa ya Tanzania ya Kidijitali (DTP) inayokusudiwa kufadhiliwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (World Bank). Lengo la Mradi pendekezwa wa DTP ni kuongeza upatikanaji wa huduma za mtandao wa Intaneti zilizo bora na kwa bei nafuu kwa serikali, wafanyabiashara na raia; na kuboresha uwezo wa Serikali kutoa huduma za umma za dijitali. Mradi wa DTP unaundwa kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda -RCIP-TZ,programu ambayo imemaliza muda wake. Utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa Awamu ya I (2021-2025) na Awamu ya Pili (2024-2029) ambazo zitashughulikia vipengele vikuu kama itakavyoelezewa katika taarifa hii. Vipengele hivi ni Ekolojia ya Dijitali, Maunganisho ya Kidijitali, Jukwaa la Huduma za Kidijitali, Usimamizi wa Miradi na Kipengele cha Kukabiliana na Dharura na majanga p. Miradi midogo midogo inapendekezwa ili kutekelezwa katika kila kipengele. Utekelezaji wa mradi wa DTP utasimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (WUUB) kwa kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB).

Vipengele vya Mradi

Mradi wa DTP umeainishwa katika vipengele vikuu vitatu vya utekelezaji ambavyo ni Ekolojia ya Dijitali, Miundombinu ya uunganishaji wa Kidijitali na Jukwaa la Huduma za Kidijitali. malengo ya vipengele hivi ni kama ifuatavyo:

- *Kipengele cha Kwanza: Ekolojia ya Kidijitali.* Lengo la kipengele hiki ni kuifanya Tanzania kuwa mahali pa kuvutia zaidi na kwenye ushindani katika uwekezaji na ubunifu wa kidijitali, kuhakikisha kuwa faida za teknolojia ya kidijitali inawafikia wananchi wengi zaidi na hivyo kusaidia kuweka msingi wa ukuaji wa uchumi wa kidijitali. Hili litatimizwa kwa kuimarisha masuala yanayohusiana na mazingira ya kustawisha ekolojia ya kidijitali yani kwa kuweka mazingira mazuri ya sheria, kanuni na sera zenye maono ya mbele; kujenga ujuzi na uwezo wa kidijitali wa taasisi na vijana; kuendeleza kundi kubwa la wabunifu, wajasiriamali, na huduma saidizi; kuendeleza tasnia imara ya TEHAMA ya ndani iliyojengeka kwa misingi ya uwekezaji binafsi na yenye uwezo wa kutoa huduma za

kufanya biashara kielektroniki, na kuondoa pengo la kidijitali ili kuhakikisha kuwa raia wote na wafanyabiashara wananufaika na maendeleo ya kidijitali. Malengo haya yatatimia kupitia:

- Mazingira wezeshi ya kidijitali.
- Miundombinu ya kusaidia maendeleo ya TEHAMA Kitaifa na kimataifa na kukuza Biashara za Kielektroniki.

- *Kipengele cha Pili: Miundombinu ya uunganishaji wa Kidijitali*. Lengo la Kipengele cha pili ni kuhakikisha kuwa Wananchi wanapata huduma za mtandao wenye kasi kubwa zaidi kwa bei ya nafuu na wa kuaminika ikiwa ni hitaji muhimu la kutoa na kupata huduma za kidijitali kwa maendeleo ya jamii pamoja na ya kiuchumi. Mbali na hatua za kuongeza ushindani katika sekta na uwekezaji wa mitandao ya kibinafsi, kuna haja ya uwekezaji wa moja kwa moja ili kukidhi mahitaji ya serikali ya kuwa na miundombinu ya uunganishwaji na pia kuweka mazingira ya kushirikiana na sekta binafsi kupeleka huduma ya mawasiliano sehemu zisizo na huduma ili kupunguza pengo la kidijitali katika utoaji wa huduma ya mtandao kati ya mijini na vijijini. Kipengele hiki kitasaidia ajenda ya serikali ya kuchochea maendeleo sawa kwa wote na kuhakikisha kuwa Wananchi wa mijini na vijijini, wanapata huduma na fursa sawa za kidijitali. Katika hili, vipengele vidogo viwili, kama inavyoonyeshwa hapa chini vitahusika:

  - Unganishwaji wa taasisi za Serikali ;
  - Mtandao wa kasi vijijini kwa ajili ya maendeleo na kuondoa pengo la Mawasiliano.

- *Kipengele cha Tatu: Jukwaa la Huduma za Kidijitali*. Lengo la kipengele cha tatu ni kuongeza uwezo wa miundombinu ya msingi inayohitajika katika utoaji wa huduma za umma za kidijitali, kuongeza ufanisi wa shughuli za ndani za serikali na kuendeleza majukwaa ya uzalishaji wa huduma za umma za kidijitali zenye vipaumbele katika ukuza uchumi na kuendeleza sekta. Kuna maendeleo yaliyofanyika katika miaka ya hivi karibuni katika kukuza huduma za kidijitali na majukwaa shirikishi ya kutolea huduma (‘mobile services portal’, ‘SMS gateway’, ‘e-payment gateway’, n.k.); kuimarishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na kuweka mifumo ya uzalishaji ya kidijitali ya Serikali (awamu ya kwanza ya Ofisi Mtandao, Mfumo wa kidijitali wa kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa mapato, n.k.). Hivyo basi kutokana na umuhimu wa Mifumo hii, serikali inalenga kuendelea na utekelezaji wa Mifumo mbalimbali kwa ajili ya kuleta huduma karibu kwa wananchi na kukuza uchumi wa kidijitali kwa kutoa fursa zaidi kwa kila mwananchi kushiriki kwenye kujenga uchumi. Kipengele hiki kitatekelezwa kupitia maeneo yafuatayo:

  - Huduma za kidijitali na Mifumo ya Uzalishaji;
  - Miundombinu ya Kuhifadhi Data; na
  - Kujenga uwezo wa kitaalamu katika masuala ya Kidijitali Pamoja na kuongeza uelewa wa matumizi ya TEHAMA kwa jamii

- *Kipengele cha Nne: Usimamizi wa Mradi*: Kipengele hiki kitahusika na usimamizi na uratibu wa shughuli za mradi.

- *Kipengele cha Tano*: *Kukabiliana na Dharura*. Kipengele hiki kitakuwa kinaweza kufadhiliwa wakati mradi unaendelea ili kuruhusu kukabili dharura zitakazo jitokeza wakati wa utekelezaji wa Mradi na zinazohitaji matumizi ya TEHAMA.

Lengo la Utaratibu wa Kuhamisha kwenye Makazi Mapya (RFP)

Lengo la RPF nikutoa mchakato wa uchunguzi, kwa shughuli za mradi wa DTP, kuhakikisha kuwa pale ambapo ardhi itahitajika kwa ajili ya shughuli za mradi, basi utaratibu wa kuhamisha kwenye makazi na fidia kwa ardhi iliyopotea, maisha na mali zingine unapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa katika namna iliyo endelevu. RPF inaweka malengo, kanuni, taratibu na njia za operesheni yoyote ya kuhamisha kwenye makazi mapya na kutoa mwongozo kwa watekelezaji kutoa fidia ya haki kwa Watu walioathiriwa na Mradi (PAPs) kwa kuzingatia Sheria za Tanzania na miongozo ya Benki ya Dunia inayosimamia fidia kwa kuhamisha wenye makazi. .

Shughuli za Mradi na Uhifadhi

Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unaopendekezwa utahusisha miradi midogo midogo, na shughuli ambazo zinaweza kuleta athari mbaya za mazingira kwenye eneo na jamii. Mpango wa Utekelezaji wa Kuhamisha kwenye Makazi Mapya (RAP) unaweza kutengenezwa ili uidhinishwe kwa kufuata kanuni za nchi . Pale ambapo uhamisho wa makazi mapya utafanyika, vifungu vinavyohusika kwenye kanuni za nchi na Sera ya Uendeshaji ya Benki ya Dunia (OP / 4.12) juu ya Uhamisho wa Makazi pasipo hiari vitatumika.

Kwa kuzingatia athari za mradi huo na kwa kuzingatia sera za uhifadhi wa mazingira na jamii za Benki ya Dunia, mradi wa DTP uliopendekezwa unawekwa kwenye Kundi B. Kuhusiana na masuala ya kuhamisha makazi, sera kuu ya uhifadhi inayoguswa ni OP / BP4.12 (Uhamisho wa Makazi pasipo Hiari).

Mpango wa Utekelezaji wa Kuhamisha kwenye Makazi Mapya (RAP) maalum zitaandaliwa zikiwa na gharama halisi wakati wa utekelzaji wa miradi midogo ambayo inaweza kusababisha kuchukuliwa kwa ardhi au uhamisho wa makazi pasipo hiari kwani, wakati mwingine, vipande vidogo vya ardhi vinaweza kuhitajika kusimika minara, vifaa vya nishati na vifaa vya mitandao ya mawasiliano. Hali halisi ya mitandao na maeneo maalum ya shughuli za mradi ambazo zinaweza kusababisha uhamisho wa makazi pasipo hiari bado haijulikani kwa wakati huu. Pale taarifa maalum za mipango zitakapopatikana na maeneo ya ardhi kutambuliwa, mipango ya uhamisho wa makazi na mipango ya fidia kwa ajili ya miradi midogo itaandaliwa kulingana na sera hii ya RPF na itawasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya idhini kabla ya uchukuliwaji wowote wa ardhi, fidia, uhamisho wa makazi mapya, au athari nyingine yoyote katika maisha haijatokea.

Uchunguzi wa miradi midogo

Miradi midogo ya Mradi wa Tanzania ya Kidijitali DTP iliyopendekezwa itafanyiwa mchakato wa uchunguzi hatua kwa hatua ili kubaini kama mradi huo mdogo utasababisha uhamishaji wa watu au adhari za kiuchumi, na hivyo kama RAP itahitajika na ikiwa ndivyo, namna ya ya kuiandaa na kuitekeleza utafanyika. Mchakato wa uchunguzi utahakikisha kuwa miradi midogo ya DTP inakidhi mahitaji ya OP 4.12 na mahitaji ya kisheria ya Tanzania kwa ajili ya ununuzi wa

ardhi. Uchunguzi wa mradi utafanyika ili kutambua aina na hali ya athari zinazoweza kuhusishwa na shughuli zilizopendekezwa za mradi wa DTP na kuweka hatua za kutosha za kushughulikia athari hizo. Uchunguzi wa masuala ya makazi mapya utakuwa sehemu ya uchunguzi wa jumla wa mazingira na jamii.

Zana ya Uhamishaji Makazi

Inatarajiwa kwamba shughuli za mradi wa DTP zitaepuka au kuzuia upatikanaji wa ardhi au kusababisha aina yoyote ya makazi mapya katika miradi midogo midogo chini ya Kipengele cha 2 na 3. Ikiwa upatikanaji wa ardhi hauwezi kuepukika, zana zifuatazo zinapaswa kutumiwa kuongoza mchakato mzima:

- Mipango ya makazi mapya;
- Mashauriano ya wadau na utoaji taarifa;
- Utafiti / sensa ya msingi ya jamii na uchumi;
- Uthamini na fidia;
- Utaratibu wa kurekebisha kero; na
- Ufuatiliaji na tathmini na ukaguzi.

Ushirikishwaji wa Wadau

Wakati wa maandalizi ya RPF hii, Mshauri Mwelekezi alifanya mashauriano kamili ya wadau kutoka watekelezaji wakuu ambao watahusika moja kwa moja na utekelezaji wa mradi wa DTP. Mashauriano hayo yalifanywa na Taasisi za Umma na binafsi zinazohusika na utekelezaji, uratibu, na uendeshaji katika ngazi ya kitaifa.

Wadau wakuu waliyoshirikishwa ni pamoja na:

(i) Wizara
- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI);
- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB);
- Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira (VPO-DoE);
- Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (WUUM);
- Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (WVBU);
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST); na
- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (WANMM).

(ii) Wakala za Serikali/au Mamlaka
- Tume ya TEHAMA (ICTC);
- Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF);
- Mamlaka ya Serikali Mtandao Agency (e-GA);
- Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL);
- Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA);
- Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA);
- Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); na
- Shirika la Posta Tanzania (TPC)

(iii) Mdhibiti wa Mazingira

- Baraza la Taifa la Menejimenti ya Mazingira. (NEMC);

(iv) Vyuo vya elimu ya juu
- Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM);
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM); and
- Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Institute of (DIT)

(v) Hospitali ya Taifa
- Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

(vi) Kampuni binafsi za mitandao
- Vodacom, Airtel, Tigo/MIC, and Halotel

(vii) Wafanyabiashara wa taka waliosajiliwa
- Chilambo General Trade Company Ltd

Hoja Kuu za Wadau

Hoja kuu muhimu za wadau hasa kuhusiana na upatikanaji wa ardhi, makazi mapya na fidia ni:

- Ubashiri wa uwepo wa ardhi kwa ajili ya kusimika miundombinu ya TEHAMA;
- Ununuzi wa ardhi unatarajiwa, lakini hakutakuwa na uhamisho kwenda makazi mapya;
- Kubadilika kwa shughuli za kujitafutia riziki kutokana na ununuzi wa ardhi;
- Fidia inapaswa kulipwa kutokana uchukuaji wa ardhi yoyote, uharibifu wa huduma zingine na vifaa, au usumbufu wa utolewaji wa huduma;
- Uwezekano wa kupoteza maisha kutokana na uharibifu wa mazao na mali nyingine;
- Uwezekano wa kupoteza miliki ya majengo ya biashara kutokana na kuhamishwa. Kwa mfano kuondolewa kwa wauzaji katika maeneo ambayo nyaya za mkongo zitapitishwa;
- Uelimishaji na uwekaji wa mipaka wa maeneo ya mradi unapaswa kufanyika ili kuepusha kuenezwa kwa uvumi wa masuala ya ardhi:
- Mradi wa DTP unaweza kufikiria kukodisha / kununua ardhi inayomilikiwa na serikali ya kijiji;
- Uelewa mdogo wa umma: jamii hazikujua kuhusu RCIP TZ; na
- Jamii zinapaswa kushirikishwa kikamilifu kutoka hatua ya usanifu hadi hatua ya utekelezaji wa mradi (ushiriki wa umma).